

# Mahudhurio ya lazima ya shule

## Maelezo kwa wazazi na walezi

Elimu kwa mtoto wako ni muhimu na mahudhurio ya kila mara shuleni ni lazima kwa mtoto wako ili kufikia ubora wao wa kielimu na kuongeza chaguzi zao za kazi na maisha. Shule za umma za NSW hufanya kazi kwa ushiriki na wazazi ili kuwatia moyo na kusaidia mahudhurio ya kila mara ya watoto na vijana. Wakati mtoto wako anapohudhuria shuleni kila siku, kujifunza kunakuwa rahisi zaidi na mtoto wako atapata na kuendeleza urafiki na watoto wengine.

## Wajibu wangu wa kisheria ni nini?

Elimu katika New South Wales ni ya lazima kwa watoto wote walio na umri wa kati ya miaka sita na chini ya umri wa chini kabisa wa kuacha shule wa miaka 17. Sheria ya Elimu ya 1990 inawahitaji wazazi wahakikishe watoto wao wa umri wa lazima kwenda shuleni wameandikishwa, na kuhudhuria shule kila mara, au wamesajiliwa na Mamlaka ya Viwango vya Elimu ya NSW kwa ajili ya shule ya nyumbani.

Wakati wanapoandikishwa, watoto wanatakiwa kuhudhuria shule kila siku ambapo ni wazi kwa wanafunzi.

## Umuhimu wa kufika kwa wakati

Kufika shuleni na darasani kwa wakati:

- huhakikisha kuwa wanafunzi hawakosi shughuli muhimu za kujifunza ambazo huratibiwa mapema asubuhi
- husaidia wanafunzi kujifunza umuhimu wa kufika kwa wakati na utaratibu
- huwapa wanafunzi muda wa kusalimiana na marafiki zao kabla ya kwenda darasani
- hupunguza usumbufu wa darasa.

Kuchelewa kunarekodiwa kama kutokuwepo kwa sehemu na lazima kuelezewe na wazazi.

## Je, itakuwaje kama mtoto wangu lazima akuwepo mbali na shule?

Wakati fulani, mtoto wako anaweza kuhitaji kutokuwepo shuleni. Sababu nzuzi kabisa za kutokuwepo kwa wanafunzi zinaweza kujumuisha:

- Kuugua, au kuwa na ugonjwa wa maambukizo
- kuwa na miadi ya matibabu isiyoweza kuepuka
- kutakiwa kuhudhuria likizo ya kidini inayotambulika rasmi
- hali ya kipekee au ya dharura ya familia k.m. kuhudhuria mazishi.

Kufuatia kutokuwepo shuleni lazima uhakikishe katika siku 7 unatoa maelezo ya mdomo au ya maandishi ya kutokuwepo kwa shule ya mtoto wako. Hata hivyo, ikiwa shule haijapata maelezo kutoka kwako ndani ya siku 2, shule inaweza kuwasiliana nawe ili kujadili kutokuwepo.

Wakuu wa shule wanaweza kukataa kukubali maelezo uliyotolewa kama hawaamini kutokuwepo ni nzuri kwa ustawi wa mtoto wako. Katika hali hizi kutokuwepo kwa mtoto wako kungeweza kurikodiwa kama bila sababu nzuri. Hii inapotokea mkuu wa shule atajadili uamuzi wake na wewe na sababu kwa nini.

Wakuu wa shule wanaweza kuomba vyeti vya kimatibabu au hati zingine wakati kutokuwepo kwa mara kwa mara au kwa muda mrefu kunaelezewa kutokana na kuwa mgonjwa. Wakuu wanaweza pia kuomba ruhusa za wazazi ili kuongea na wataalum kupata habari ili kutengeneza mpango wa afya wa kusaidia mtoto wako. Ikiwa ombi lile linakataliwa, mkuu anaweza kurekodi kutokuwepo kuwa bila sababu nzuri.

## Usafiri

Familia zinatiwa moyo kusafiri wakati wa likizo za shule. Ikiwa kusafiri wakati wa kipindi cha shule ni lazima, zungumza hii na mkuu wa shule ya mtoto wako. Ombi la Likizo ya Kurefusha linaweza kuhitajika kukamilishwa. Kutokuwepo kunachohusu kusafiri kutarekodiwa kama likizo kwenye orodha ya mahudhurio na kwa hiyo kutahesabiwa katika jumla ya kutokuwepo kwa mtoto wako kwa mwaka ule.

Katika hali fulani wanafunzi wanaweza kustahiki kuandikishwa kwa elimu ya mbali kwa vipindi vya kusafiri vya zaidi ya siku 50 za shule. Hii inapaswa kujadili na mkuu wa shule ya mtoto wako.

## Mtoto wangu hataenda shule, nifanyeje?

Unapaswa kuwasiliana na mwalimu mkuu haraka iwezekanavyo ili kujadili suala na kuomba msaada. Mikakati ya kusaidia kuboresha kuhudhuria inaweza kujumuisha mwelekezo kwa timu ya shule ya kujifunza na usaidizi au kuunganisha mtoto wako na mitandao ya kuunga mkono inayofaa. Mwalimu mkuu anaweza kupata usaidizi zaidi kutoka Mpango wa Uwasiliano wa Nyumbani na Shule ili kuunda Mpango wa Kuboresha Mahudhurio.

## Ni nini kinachoweza kutokea ikiwa mtoto wangu anaendelea kutokuwepo kusikokubalika?

Ni muhimu kuelewa kwamba Idara ya Elimu inaweza kuhitajika kuchukua hatua zaidi ambapo watoto wa umri wa lazima kwenda shuleni wana idadi inayorudia ya kutokuwepo bila maelezo au sababu nzuri kutoka shuleni.

Baadhi ya hatua inayofuata inaweza kuchukuliwa:

- Mikutano ya Lazima ya Shule

Unaweza kuulizwa, pamoja na mtoto wako, kuhudhuria Mkutano wa Lazima wa Shule. Mkutano ule utasaidia kutambulia misaada ambayo mtoto wako anaweza kuhitaji ili ahudhurie shule kila mara. Shule, wazazi na mashirika yatashirikiana pamoja kuunda mpango wa kukubaliwa (kujulikana kama Ahadi) ili kusaidia mtoto wako kuhudhuria shuleni.

- Ombi kwa Mahakama ya Watoto – Agizo la Lazima la Shule

Ikiwa mahudhurio ya mtoto wako shuleni yanaendelea kutoridhika Idara ile inaweza kuomba kwa Mahakama ya Watoto kupata Agizo la Lazima la Shule. Mhakimu wa Mahakama ya Watoto anaweza kuagiza Mkutano wa Lazima wa Shule kufanyikiwa.

- Kushtakiwa kwenye Mahakama ya Mtaa

Wafanyakazi wa Shule na Idara huahidi kushughulikia kwa ushiriko nawe ili kukabili na masuala yanayozuia ushirikiano mzima wa mtoto wako shuleni. Katika hali ambapo uvunjaji wa maagizo ya lazima ya shule unatokea hatua zaidi inaweza kuchukuliwa dhidi ya mzazi katika Mahakama ya Mtaa. Matokeo ya matendo ya mahakama yanaweza kuweka agizo la huduma ya jamii au faini.

## Je, mtoto wangu anaweza kuacha kwenda shule kwa umri gani?

Wanafunzi wote wa New South Wales lazima wakamilishe Mwaka wa 10 au usawa wake. Baada ya Mwaka wa 10, na hadi wanapofikia umri wa miaka 17, kuna uchaguzi mbalimbali wa kubadilika rahisi kwa wanafunzi kukamilisha elimu yao.

## Kufanya kazi kwa ushirikiano

Idara ya Elimu ya NSW hutambua kwamba kushughulikia pamoja na wanafunzi na familia zao ni njia nzuri sana kusaidia mahudhurio ya kila mara ya wanafunzi shuleni.

Tunatarajia kushughulikia kwa ushirikiano nawe kumsaidia mtoto wako kutimiza fursa za maisha yake.

## Huduma ya mkalimani wa simu

Tafadhali wasiliana na shule Ikiwa ungetaka kupata habari zaidi. Ikiwa unahitaji usaidizi wa mkalamani ili kuwasiliana na shule, tafadhali piga simu kwa 131 450, uwaambie unahitaji lugha gani na uliza mpigaji simu kupita simu kwa shule. Mwendeshaji simu atapata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia na mazungumzo yako. Hutatozwa kwa huduma hii.